HESLB
BODI YA MIKOPO
TUNAWEKEZA KWA KIZAZI CHA BAADAE

# MASWALI NA MAJIBU

## KUHUSU UOMBAJI MIKOPO

## 2022/2023

Yanapatikana
**www.heslb.go.tz**

#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

HESLB TANZANIA HESLB_TANZANIA

1. **Swali:** Je, ni wakati gani naweza kuomba mkopo wa elimu ya juu?

**Jibu:** Maombi ya mkopo hufanyika mara moja kwa mwaka wa masomo. Kwa mwaka 2022/2023, maombi yataanza kupokelewa kwa njia ya mtandao kuanzia Julai 15 hadi Septemba 30, 2022.

2. **Swali:** Zipi ni sifa kuu za kupata mkopo wa elimu ya juu?

**Jibu:** Mwombaji wa mkopo anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:
- Awe mtanzania;
- Awe ameomba mkopo kwa njia ya mtandao kama inavyoelekezwa;
- Awe amepata udahili (admission) uliothibitishwa kwenye chuo kinachotambuliwa;
- Asiwe na chanzo kingine cha kugharamia masomo yake ya elimu ya juu kama ufadhili mwingine, ZHELB n.k;
- Aidha, mwombaji anashauriwa kusoma maelezo ya kina kuhusu sifa na vigezo hutolewa kwenye Mwongozo wa Utoaji Mikopo unaopatikana katika tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz)

3. **Swali:** Je, yatima na wenye ulemavu yanapewa kipaumbele katika uombaji mikopo?

**Jibu:** Pamoja na sifa kuu, upangaji mikopo pia hutoa kipaumbele kwa makundi maalum kama waombaji yatima, wenye ulemavu au wenye wazazi wenye ulemavu, na wanafunzi waliofadhiliwa katika masomo ya sekondari kutokana na kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama za elimu.

Waombaji mikopo kutoka makundi haya wanapaswa kusoma Mwongozo wa Utoaji Mikopo kwa mwaka 2022/2023 unaoelekeza mambo muhimu ya kuzingatia na nyaraka zinazotakiwa.

4. **Swali:** Ninapaswa kufanya nini ili niweze kuanza kuomba mkopo kwa njia ya mtandao (OLAMS)?

**Jibu:** Soma mwongozo unaotolewa na HESLB ambao unapatikana katika tovuti ya Bodi (www.heslb.go.tz), kisha, fungua mtandao wa maombi (olas.heslb.go.tz) ili ujisajili kwa kutumia namba yako ya mtihani wa kidato cha nne na mwaka uliofanya mtihani huo.

5. **Swali:** Baada ya kujisajili, napaswa kufanya nini?

**Jibu:** Baada ya kujisajili, utapata namba ya kumbukumbu (Control Number) kwenye 'screen' ambayo itakuwezesha kufanya malipo ya ada ya maombi ya TZS 30,000/= kwa njia ya benki au simu. Lipa mara moja tu kiasi kamili cha TZS 30,000/=

6. **Swali:** Ni nyaraka gani muhimu zinatakiwa wakati wa kuomba mkopo?

**Jibu:** Nakala za:

i. Cheti cha kuzaliwa cha mwombaji kilichothibitishwa na RITA au ZCSRA;
ii. Stashahada (Diploma) kwa waombaj waliohitimu stashahada;
iii. Cheti cha kifo ikiwa umepoteza mzaz kilichothibitishwa na RITA au ZCSRA;

iv. Kitambulisho cha mdhamini (NIDA, Mpiga Kura, Leseni ya Udereva, Pasi ya Kusafiria au kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi). Mdhamini anaweza kutumia kimoja kati ya vitambulisho hivi;
v. Fomu ya ufadhili iliyojazwa kikamilifu na kusainiwa ikiwa mwombaji alifadhiliwa katika masomo yake sekondari au stashahada;
vi. Kwa wenye ulemavu au wenye wazazi wenye ulemavu, fomu maalum iliyojazwa kikamilifu na kuthibitishwa na Mganga Mkuu wa Wilaya;
vii. Picha (passport size) za mwombaji wa mkopo na mdhamini wake (mdhamini anaweza kuwa mzazi au mlezi).

**7. Swali:** Je, kuna umuhimu wa kuwa na Akaunti ya Benki au Namba ya NIDA wakati wa kuomba mkopo?

**Jibu:** Ndiyo. Mwombaji mkopo anashauriwa na kusisitizwa kuwa na Akaunti yake ya Benki ili kurahisisha malipo akifika chuoni. Mwombaji anaweza kufungua akaunti katika benki yoyote aipendayo ila majina ya akaunti ya benki yawe sawa na majina anayotumia kuomba mkopo.

Kuhusu namba inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), mwombaji anashauriwa kuiweka (kama anayo). Kama hana, anaweza kuendelea na maombi bila namba hiyo.

**8. Swali:** Je, mwanafunzi anaweza kupata usaidizi wa kuomba mkopokwenye 'Internet Café'?

**Jibu:** Ndiyo. Hata hivyo, unashauriwa kuhakikisha kuwa taarifa zako zimejazwa kwa usahihi. Ni wajibu wa mwombaji mkopo kuhakikisha viambatanisho vyote (vyeti na nyaraka nyingine) vimewekwa/vimepakiwa kwenye fomu yake mtandaoni ili kuepuka maombi yake kuwa na upungufu.

**9. Swali:** Je, ni wapi nitahakiki cheti za kuzaliwa au kifo cha mzazi?

**Jibu:** Vyeti vya kuzaliwa na vya vifo vya wazazi lazima vihakikiwe na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) au ZCSRA (kwa Zanzibar) kabla havijapakiwa (uploaded) kwenye mfumo wa maombi ya mkopo wa HESLB. taasisi hizi katika kufanya uhakiki wa vyeti.

**10. Swali:** Iwapo niliwahi kupata mkopo zamani na nikaacha, kushindwa au kufukuzwa chuo, nitaweza kupata mkopo mwingine?

**Jibu:** Lengo la mikopo ya elimu ya juu ni kumuwezesha mwanafunzi kusoma na kumaliza masomo kwa wakati. Hivyo, iwapo uliwahi kuwa mnufaika wa mkopo wa fedha za Serikali, na hukumaliza masomo, utapaswa kwanza kurejesha mkopo wote au angalau asilimia 25 ya deni lako kabla ya kufikiriwa kupata mkopo mwingine.

**11. Swali:** Kama nina wazazi wasio na uwezo, je niwasilishe uthibitisho wa aina gani ili kupata mkopo?

**Jibu:** Mwombaji ambaye ana mahitaji maalum, ni lazima mahitaji na hali yake ithibitishwe na mamlaka husika kama Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) au taasisi za aina hiyo zinazotambulika na zinazoweza kuthibitisha.

**12. Swali:** Kama nilikosa mkopo mwaka jana, nikalazimka kuahirisha masomo, natakiwa kuomba tena mkopo mwaka huu?

**Jibu:** Unaruhusiwa kuomba upya mkopo mwaka huu. Maombi yako yatapimwa kwa mwongozo na vigezo vya mwaka huu wa masomo. Unashauriwa usome mwongozo kwa makini na kuuzingatia.

Aidha, kama unasoma mwaka wa pili au wa tatu na kuendelea na una uhitaji wa mkopo, unaruhusiwa kuomba kwa kuzingatia vigezo vya mwaka huu.

**13. Swali:** Fomu za maombi ya Mikopo zinawasilishwaje HESLB?

**Jibu:** Baada ya kuzi-upload na kukamilisha kujaza fomu ya maombi, mwombaji a-print fomu iliyokamilika na kuituma kwa EMS kwenda kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
S.L.P. 76068,
15471 DAR ES SALAAM.

**14. Swali:** Mwombaji atajuaje iwapo amepata mkopo?

**Jibu:** Baada ya HESLB kupokea, kuhakiki na kuchambua maombi ya mikopo, taarifa kwa watakaofanikiwa kupangiwa mikopo itapatikana kwenye tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz), vyuoni na kwenye akaunti za waombaji mikopo.

**15. Swali:** Je, mwombaji anawezaje kufuatilia taarifa za maombi yake ?

**Jibu:** Kuanzia mwaka 2019/2020, waombaji mkopo na wanafunzi wanufaika wa mkopo waliopo vyuoni wanaweza kufuatilia mwenendo na taarifa zao kupitia akaunti yake ya SIPA (Student's Individual Permanent Account).

Hii ni akaunti ambayo mwombaji ametumia kuomba mkopo na ataendelea kuitumia kupata taarifa mbalimbali hata akiwa chuoni.

**16. Swali:** Mkopo unatolewa kwenye vipengele (Loan Items) vipi?

**Jibu:** Mwombaji mkopo aliyekidhi vigezo na sifa, anaweza kupangiwa vyote au baadhi ya vipingele vifuatavyo kutokana na uhitaji wake:

- Chakula na malazi
- Ada ya mafunzo
- Vitabu na viandikwa
- Mahitaji maalumu ya kitivo
- Utafiti
- Mafunzo kwa vitendo

Imetolewa na:
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
info@heslb.go.tz
Julai, 2022

## Uombaji Mikopo
## 2022/2023

**TAREHE MUHIMU**

**Julai 15 - 18 2022**
Waombaji kusoma Mwongozo
katika www.heslb.go.tz

**Julai 15 - Septemba 30 2022**
Mfumo wa kuomba mkopo
www.olas.heslb.go.tz
kuwa wazi

**Septemba 30, 2022**
Mfumo kufungwa

**#WeweNdoFuture | #TimizaWajibu**

HESLB TANZANIA HESLB_TANZANIA